**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 9, Issue 1, 2026**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usimulizi kama Kipengele cha Muundo Unavyojitokeza kwenye Diwani ya Akiba ya Wema Iliyohaririwa na Timothy Arege

*Reuben Wahome Muthoni[1*] na Dkt. Jesse Joseph Muriithi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu Cha Kenyatta, S.L.P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID; https://orcid.org/; 0009-0001-0653-0761; Barua pepe ya mawasiliano wahomemuthonij@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*23 Januari 2026*

**Istilahi Muhimu**:

*Usimulizi, Diwani ya Akiba ya Wema, Sauti za usimuliaji, Viwango vya usimulizi, Uendelezaji wa hadithi.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza usimulizi kama kipengele cha muundo kwenye Diwani ya Akiba ya Wema ambayo imehaririwa na Timothy Arege. Malengo ya utafiti huu yalikuwa pamoja na kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi vinavyotumika katika Diwani ya Akiba ya Wema iliyohaririwa na Timothy Arege, Kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi wa hadithi kwenye diwani hii, kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa hadithi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Naratolojia ambayo ilianzishwa na mwasisi Plato na baadaye kuendelezwa na wengine kama: Propp (1968), Claude (1970), Barthes (1975), Todorov (1977), Genette (1980), Bal (1999) na Fludernik (2009). Nadharia hii hutumika kuchunguza jinsi matukio hufuatana kwenye hadithi fulani. Utafiti huu ulichunguza usimulizi kwa nadharia hii kuegemea mwelekeo wa Genette (1980). Vigezo vya nadharia hii vilivyozingatiwa ni sifa za muundo wa usimulizi na vipengele vyake kuzingatia uamilifu au uhusiano uliopo kiwakati na kiusemi. Utafiti ulikuwa umejikita maktabani ambapo, vitabu, majarida, tasnifu na makala ambayo yanahusu usimulizi yalisomwa. Mbinu ya usampulishaji makusudi ilitumika katika kukusanya data iliyotokana na waandishi tofauti kuhusu usimulizi. Asilimia 40 ya sampuli kuhusu usimulizi ilitumika kwenye hadithi ambazo ni 13 hivyo hadithi 5. Mafungu yanayoonyesha fikra za wahusika na miundo mbali mbali ya hadithi mahsusi yalidondolewa kwenye sampuli ya hadithi tano zilizochaguliwa.

**APA CITATION**

Muthoni, R. W. & Muriithi, J. J. (2026). Usimulizi kama Kipengele cha Muundo Unavyojitokeza kwenye Diwani ya Akiba ya Wema Iliyohaririwa na Timothy Arege. *East African Journal of Swahili Studies*, *9*(1), 48-57. https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

**CHICAGO CITATION**

Muthoni, Reuben Wahome and Jesse Joseph Muriithi. 2026. “Usimulizi kama Kipengele cha Muundo Unavyojitokeza kwenye Diwani ya Akiba ya Wema Iliyohaririwa na Timothy Arege”. *East African Journal of Swahili Studies* 9 (1), 48-57. https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

**HARVARD CITATION**
Muthoni, R. W. & Muriithi, J. J. (2026) "Usimulizi kama Kipengele cha Muundo Unavyojitokeza kwenye Diwani ya Akiba ya Wema Iliyohaririwa na Timothy Arege", *East African Journal of Swahili Studies*, 9(1), pp. 48-57. doi: 10.37284/jammk.9.1.4383

**IEEE CITATION**
R. W., Muthoni & J. J., Muriithi "Usimulizi kama Kipengele cha Muundo Unavyojitokeza kwenye Diwani ya Akiba ya Wema Iliyohaririwa na Timothy Arege", *EAJSS*, vol. 9, no. 1, pp. 48-57, Jan. 2026.

**MLA CITATION**
Muthoni, Reuben Wahome & Jesse Joseph Muriithi. "Usimulizi kama Kipengele cha Muundo Unavyojitokeza kwenye Diwani ya Akiba ya Wema Iliyohaririwa na Timothy Arege". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 9, no. 1, Jan. 2026, pp. 48-57, doi:10.37284/jammk.9.1.4383.

## UTANGULIZI

Kutokana na uchunguzi wa awali wa mtafiti kulikuwa na pengo la utafiti kuhusu hadithi fupi haswa usimulizi kama kipengele cha muundo. Hata hivyo kuna tahakiki nyingi ambazo zimeandikwa kuhusu usimulizi kama kipengele cha muundo ndani ya riwaya ya Kiswahili na ndani ya kazi za kishairi miongoni mwa kazi nyingine. Hata hivyo ni kazi chache ambazo zinahakiki usimulizi kama kipengele cha muundo kwenye hadithi fupi. Fisher (1984) alifanya utafiti kuhusu usimulizi kama njia ya mazungumzo. Aligundua kuwa binadamu hujenga maisha yao kwa njia ya hadithi wanazosimulia kuhusu maisha yao ya kila siku. Alichambua jinsi wasimuliaji wanavyoelekeza hadithi zao kwa hadhira hai, wakilenga masuala ya kijamii na kuunda hadithi zenye mpangilio na ujumbe maalum. Alikuja kugundua kwamba mbinu ya usimulizi ni muhimu katika kufikisha ujumbe kwa ufanisi. Matokeo ya utafiti wake yalikuwa ya muhimu kwa sababu yalitoa ufahamu wa kina kuhusu usimulizi katika mazungumzo na pia kuchunguza njia mbalimbali za usimulizi zilizotumiwa katika mwandishi maalum.

Msokile (1993), katika ufafanuzi wake kuhusu usimulizi, anaelezea simulizi kama maelezo ya tukio fulani yanayosimuliwa na msimulizi. Anaeleza kuwa simulizi ni aina ya mazungumzo ambapo msimulizi anatoa maelezo na mawazo kuhusu matukio katika hadithi. Msokile anaelezea kwamba hadithi inaweza kuwa na mpangilio wa wakati ambao si wa moja kwa moja, na inaweza kuwa na muundo wa nyuma na mbele. Pia, anabainisha umuhimu wa wahusika katika hadithi na kuwatambua kama wahusika wakuu na wadogo, hivyo kuonyesha umuhimu wa kuchunguza riwaya na mbinu za usimulizi.

Kuhusu vijengo vya riwaya, Mohamed (1995) anaeleza kuwa hadithi hujengwa kupitia sauti ya msimulizi, na msimulizi hutumia mbinu mbalimbali kulingana na mahitaji yake. Anaelezea mbinu kama usimulizi wa nafsi ya kwanza ambapo msimulizi anaweza kuwa mshiriki wa matukio au asiwe mshiriki, na usimulizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi haelezi matukio yanayomhusu yeye binafsi. Mohamed pia anabainisha aina za wahusika kama vile wahusika mviringo, bapa na kinyago, ambazo zinaathiri jinsi hadithi inavyosimuliwa. Maandishi haya yalisaidia katika utafiti kuchunguza uwezekano wa wahusika na mbinu za usimulizi katika maandishi husika.

Gaita (1998), alitathmini namna usimulizi ulikuwa umejitokeza kwenye Riwaya za Kezilahabi na za Said A. Mohammed. Utafiti huu uliibua dhana kuwa palikuwa na uhusiano mkubwa baina ya muundo na maudhui. Alitathmini namna uwasilishaji wa hadithi fulani kimuundo ulivyotegemea maudhui yaliyokuwepo kwenye utafiti huu akiitumia nadharia ya Naratolojia atika kutathmini hili. Utafiti huu ulilenga zaidi mahusiano ya usimulizi kama kipengele na maudhui. Vipengele vya usimulizi havikugusiwa hivyo. Vilevile utafiti huu ulitafiti riwaya ya Kiswahili. Utafiti lengwa unanuia kuchunguza sauti za usimulizi na viwango vyake vilivyotumika. Aidha, mtafiti atalenga kuonyesha nafasi katika usimulizi katika uwasilishaji wa usemi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

na fikra za mhusika. Japo matini hii haijataja viwango hivyo, kazi hii imetumia nadharia ya Naratolojia itakayotumika katika utafiti huu.

Njogu na Chimerah (1999) wanadefini usimulizi kama sauti ya kueleza hadithi na wanabainisha aina kadhaa za usimulizi. Wanagundua kwamba aina moja ya usimulizi ni ile ambapo mwandishi hutumia nafsi ya tatu na anakuwa na uhuru mkubwa katika uandishi. Hii ni kawaida sana katika fasihi ya Kiswahili. Aina nyingine ni ile ambapo wahusika wanasimulia matendo yao na ya wenzao, huu ukifahamika kama usimulizi wa mazungumzo. Maelezo yao yalikuwa muhimu katika utafiti wao kwa kubaini aina za usimulizi katika riwaya trilojia ya Siri Sirini. Kwa upande wake, Bal (2004) anaeleza kwamba msimulizi anaweza kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi, kama vile nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Anasisitiza kuwa urefu wa hadithi unaweza kusababisha mpangilio wa ki-anakroni ambapo matukio yanaweza kurudiwa au kuwa na mzunguko. Maelezo yake yalichangia katika kutoa ufahamu zaidi kuhusu usimulizi katika utafiti huo.

Mohochi (2000) anaamini kwamba usimulizi ni msingi muhimu katika uwasilishaji wa kazi za fasihi, hasa nathari. Anaona usimulizi wa nafsi ya kwanza kama muhimu, ambapo msimulizi hutoa maelezo ya kina kuhusu wahusika na matukio ya kihistoria Ong`ondi (2005), alishughulikia usimulizi kwenye *Riwaya ya Walenisi* ya Katama Mkangi. Kwenye uchambuzi wake vipengele vilivyoshughulikiwa ni kama vile, mtazamo wa msimulizi, sauti ya msimulizi kiwakati na mpangilio wa hadithi aidha aliangazia mpangilio wa hadithi kwenye sehemu yake ya utafiti alifanikiwa kushughulikia kwa kiasi kikubwa Riwaya. Japo utafiti huu ulishughulikia mada ya usimulizi, vipengele vilivyoshughulikiwa vilikuwa vichache na hivyo utafiti lengwa utapanua mawanda kwa kushughulikia vipengele zaidi vya wakati na usemi na fikra za wahusika. Matini hii imetumia vipengele ambavyo vitafaa itafiti lengwa vya sauti ya usimulizi na hivyo mtafiti utamfaa. Utafiti lengwa utashughulikia hadithi fupi. Vipengele alivyotumia kutafitia usimulizi vinawiana na baadhi ya vile ambavyo mtafiti amechagua kuvitumikiza.

Arege (2012), aliangazia usimulizi kwenye ushairi wa Kiswahili kurejelea *Uteuzi wa Rasi' Lghuli* kwenye tasnifu yake ya Uzamifu. Kwenye tasnifu yake aliangazia viwango vya usimulizi kwenye ushairi wa Kiswahili na pia sauti aidha kwenye tasnifu yake aliangazia usimulizi zongomezi na usimulizi baadaye. Aidha aliangalia mapito ya kiwakati kwa kurejelea nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu pia vilijadiliwa, vilevile aliangazia metalapsi yaani mpito wa simulizi kwa viwango tofauti tofauti vya usimulizi. Arege (2012), alichunguza mbinu za usimulizi kwa kurejelea usimulizi baadaye, usimulizi kabla, usimulizi zongomezi na vilevile usimulizi ambao ni mseto .Hili litakuwa lina uwiano na lengo langu la kuchunguza viwango vya usimulizi kiwakati, japo Arege alichunguza Utenzi wa Kiswahili. Tofauti na utafiti wa awali mtafiti ananuia kuchunguza hadithi fupi za Kiswahili haswa diwani ya *Akiba ya Wema*, iliyohaririwa na Arege Timothy. Mtafiti analenga utakuwa unaangazia mapito ya wakati katika usimulizi na kulenga pia sauti za usimulizi. Hili ni sawia na utafiti huu ambao uliangazia mapito ya wakati katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu wa Timothy Arege utatoa mwangaza wa kuongoza mtafiti katika kufanya utafiti na kutafitia vipengele sawia na vyake vya usimulizi.

Kinara (2012), alichunguza usemi ulivyotumika katika kusawiri mambo yanayohusiana na ukimwi. Kwenye matini yake japo hakutaja usimulizi, sauti ya usimulizi ilitegemewa sanana kurejelewa mara kwa mara. Kazi hii ya Kinara japo ilirejelea usemi sana, ilitumia nadharia ya Naratolojia katika utafsiri wake. Hivyo utafiti huo wake utamfaa mtafiti haswa kipengele cha usimulizi na kubainisha sauti ya msimulizi katika kazi yake ya utafiti kimetumika katika kubainisha usimulizi na kipengele cha usemi wa wahusika katika Riwaya teule.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

Shitemi (2012), alitafiti usimulizi kwenye utenzi, alirejelea utenzi wa *Siri la Asiraili*. Katika utafiti huu wake aliangazia sifa za kimuundo kwa kurejelea usimulizi kwenye utenzi wa Kiswahili. Alisheheni kuwa sifa za kiusimulizi ambazo hujitokeza katika Riwaya vilevile zilikuwa kwenye utenzi wa Kiswahili. Shitemi alibaini vipengele vya naratolojia kama vile hadithi, matini na usimulizi kisauti. Utafiti huu wa Shitemi utamfaa mtafiti ama vile ametafiti vipengele ambavyo vimetokana na nadhania ambayo ninaitumia ya naratolojia. Naratolojia inabainisha vipengele vya usimulizi ambavyo vimejitokeza wazi kwa kazi yake. Nitatumia vipengele vivyo hivyo vitatumika kwenye utafiti lengwa kwa kiasi kikubwa.

Nyambane (2013), alitafiti kuhusu uchanganuzi na uchambuzi wa matumizi ya lugha katika riwaya na Hadithi fupi za Clara Momanyi. Katika utafiti huu alitumia nadharia ya Elimu-mtindo katika kuchanganua jinsi lugha inavyotumika kifasihi katika riwaya na Hadithi fupi za Clara Momanyi. Aligundua kuwa japo mtindo wa uwasilishaji wa hadithi fupi ulifuata na kuchagua maneno yaliyonuiwa kumulika msomaji kwa kiasi kikubwa, usimulizi ulijitokeza kwa kiasi kikubwa na hata kupelekea hadithi fupi alizotafiti za Clara Momanyi kuwa na nadhari katika kuwasilisha mawazo yake Aidha, aligundua kuwa nathari ya usimulizi wa hadithi ilikuwa muhimu sana katika utambuzi wa hadithi tofauti tofauti na kupelekea kuwa na maono au mwelekeo wa kiriwaya kwa kiasi kikubwa. Utafiti huu utamfaa mtafiti kwa vile umechambua hadithi fupi kilugha na kimtindo na kuzingatia vipengele vya usimulizi kama vile sauti ya msimulizi na viwango vyake, kipengele hiki nanuia kukitumia kwa kurejelea kazi hii.

Omutimba (2015), alihakiki usimulizi katika Riwaya na kurejelea *Riwaya ya Adili ya nduguze*. Katika utafiti wake alilenga kutathmini ikiwa riwaya za Kiswahili zina miundo maalum ya fomula inayotumiwa kuendeleza usimulizi wake. Hata hivyo ,malengo ya utafiti wake ni tofauti na anachokusudia mtafiti wa vile yeye alikusudia kuonyesha vigezo na sifa tofauti kwenye Riwaya tatu tofauti. Hata ingawaje alitafitia usimulizi ambao mtafiti ananuia kutafitia, nadharia aliyotumia ni ya Muundo na Maumbo Tengamano. Hata hivyo kurejelea usimulizi kwake kutanifaa kwa kiasi kikubwa haswa kufafanua mada.

Mwongela (2021), alitafiti kuhusu usimulizi kwenye Riwaya Trilojia ambapo mifumo aliyotumia wenye *Riwaya ya Siri Sirini*. Kulingana na utafiti huu ulioangazia Riwaya hii iliyoandikwa na Rocha Chimerati ilikuwa imetumia vipengele muhimu na tofauti vya usimulizi kama vile hotuba, usimulizi penyezi, tautolojia, motifu ya safari, nyimbo, kirejeshi, elekezi, muhtasari udondoshi na nyingine. Usimulizi huu ni taa inayoongoza utafiti ninaonuia kufanya haswa vipengele vya usimulizi. Viwango vya usimulizi ambavyo ametafitia vitafaa utafiti lengwa kwa vile ni mojawapo vya vipengele lengwa. Hata hivyo usimulizi huu ulijikita kwenye Riwaya ya Trilojia ila huu utajikita kwa Diwani ya hadithi fupi.

Pengo linaloonekana kati ya tafiti zilizotajwa ni kwamba wengi wa watafiti waliotafiti usimulizi wamejikita katika riwaya au utenzi, huku usimulizi katika diwani ya hadithi fupi ukipuuzwa kwa kiasi kikubwa. Watafiti kama Gaita (1998), Ong'ondi (2005), na Arege (2012) walilenga riwaya na utenzi, wakitumia nadharia za Naratolojia na Muundo, lakini hawakuchuguza kwa kina viwango vya usimulizi na sauti za wahusika kwenye hadithi fupi. Hivyo, utafiti lengwa ulileta upya mtazamo kwa kuchunguza vipengele hivi kwenye diwani ya hadithi fupi ya *Akiba ya Wema*, na kujaza pengo lililoachwa kwenye tafiti zilizotangulia.

## MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu unahusisha uchunguzi wa mbinu za usimulizi katika Diwani ya *Akiba ya Wema*, ukitumia mwongozo wa nadharia ya **Naratolojia**. Nadharia hii, ambayo imejikita katika misingi ya Umuundo, huchambua muundo wa simulizi kwa kuligawanya katika vipengele vyake na kuchunguza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

jinsi vinavyoshirikiana ili kutimiza dhima zao. Kulingana na **Genette (1980)**, Naratolojia hutoa vigezo vinavyosaidia katika ukaguzi wa simulizi kwa kuangazia vipengele vya ndani kama vile mpangilio wa hadithi, mbinu za usimulizi, mitazamo inayojitokeza, mazungumzo na fikra za wahusika, pamoja na kipengele cha wakati.

**Historia ya Nadharia ya Naratolojia**

Mawazo ya Naratolojia yana asili yake katika maandishi ya mwanafalsafa wa Kiyunani, **Plato (428-348 KK)**, hasa katika kazi yake **"The Republic"**. Hata hivyo, nadharia hii ilianza kukomaa kupitia **Nadharia ya Muundo ya Kirusi** iliyoanzishwa na **Vladimir Propp (1968)**. **Todorov (1971)** aliitafsiri Naratolojia kama taaluma inayohusika na masimulizi na miundo yake, akisisitiza umuhimu wa matukio ya kijamii na mfumo wa jamii husika. **Barthes (1977)** aliona Naratolojia kama mfumo wa kuchunguza jinsi hadithi zinavyoundwa, akisisitiza kuwa kila hadithi inajengwa na miundo ya kina ambayo ni ya ulimwengu wote. Mchango mkuu wa **Gérard Genette (1980)** katika kazi yake **"Narrative Discourse"** uliimarisha nadharia hii kwa kuchambua kwa kina jinsi simulizi inavyowasilishwa na kuunda maana.

**Mihimili ya Nadharia ya Naratolojia kwa Mujibu wa Gérard Genette**

Utafiti huu uliendelezwa kwa misingi ya Genette, ambayo ilitoa mfumo wa kina wa kuchambua hadithi. Ulianza kwa kuzingatia **Sauti ya Usimulizi**, ambao ulichunguza "nani alisema" na "wakati alisema". Huu ulihusisha kama msimulizi alikuwepo ndani ya matukio au la. Aina mbalimbali za wasimulizi zilichunguzwa, kuanzia yule aliyesema kwa nafsi ya kwanza, hadi yule aliyekuwa anajua kila kitu kuhusu wahusika. Wataalamu mbalimbali, kama Bonheim na Mieke Bal, walieleza jinsi sauti ya msimulizi iliweza kuathiri jinsi msomaji alivyopokea hadithi.

Utafiti pia ulichunguza **Viwango vya Usimulizi**, ambavyo viliruhusu msomaji kutofautisha kati ya hadithi kuu na zile ndogo zilizokuwemo ndani yake. Hapa, maneno kama "ndani ya hadithi" na "hadithi ndani ya hadithi" yalitumiwa kuelezea viwango hivi. Viwango hivi vilikuwa muhimu kwa kuwa viliathiri jinsi hadithi ilivyopokelewa, na vilisaidia kuelewa miundo ya hadithi.

Mhimili wa **Wakati wa Usimulizi** uliangalia uhusiano kati ya muda wa matukio katika hadithi na muda uliotumiwa kueleza matukio hayo. Vipengele vitatu vikuu vilichunguzwa: **Mpangilio**, ambao ulihusisha jinsi matukio yalivyopangwa, ikiwemo matumizi ya kurudisha nyuma au kusonga mbele katika muda. Kisha kulikuwa na **Muda**, ulioangalia uhusiano kati ya urefu wa tukio na muda uliotumiwa kulieleza. Mwisho kulikuwa na **Marudio**, yaliyoonyesha jinsi matukio yalivyokuwa yakirudiwa katika hadithi.

Hatimaye, utafiti huu ulijikita katika jinsi **Fikra na Mawazo ya Wahusika** yalivyowasilishwa. Hii ilikuwa muhimu kwa kufichua hisia na mielekeo ya wahusika. Mbinu mbalimbali, kama vile kunukuu maneno ya mhusika moja kwa moja, au kutumia msimulizi kueleza mawazo ya mhusika, vilichunguzwa. Pia, matumizi ya "uzungumzi nafsia" yalionyesha hali ya ndani ya mhusika. Kwa ujumla, nadharia hii ilisaidia kueleza jinsi uhalisia wa hadithi ulivyoundwa na kuifanya ivutie zaidi.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia mbinu ya maktabani, ambapo vitabu, majarida, na tasnifu zilizohusu usimulizi zilisomwa na kuchambuliwa. Sampuli ya hadithi tano kati ya kumi na tatu kutoka kwenye diwani ya *Akiba ya Wema* iliteuliwa kimakusudi. Hadithi hizi ni:

- *Damu ya Baba* – Nicholas O. Otieno
- *Sifa wa Mwakiwiwi* – Francis Macharia
- *Akiba ya Wema* – Abdulrahman Kitingi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

- *Luka Semagongo* – Fredrick M. Masese
- *Mabega ya Mkurugenzi* – Timothy M. Arege

Uchanganuzi ulifanywa kwa kutumia mihimili ya Nadharia ya Naratolojia ya Genette, na matokeo yalipangwa kulingana na malengo ya utafiti.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Ilidhihirika kuwa Hadithi fupi; *Damu ya Baba* iliyoandikwa na Nicholas O. Otieno, *Sifa wa Mwakiwiwi* iliyoandikwa na Francis Macharia, *Akiba ya Wema* iliyoandikwa na Abdurahman Kitingi, *Luka Semagongo* iliyoandikwa na Fredrick M Masese na *Mabega ya Mkurugenzi* iliyoandikwa na Timothy M Arege zilizo kwenye Diwani ya *Akiba ya Wema na Hadithi Nyingine* zimehusisha sifa na mitazamo ya usimulizi kwenye uwasilishaji wake.

Hadithi fupi zilizochambuliwa zilihusisha aina mbili za wasimulizi, msimulizi wa ndani na wa nje. Aghalabu, msimulizi wa ndani huonekana wazi na kujulikana na msomaji kwani anahusika kwenye matukio anayosimulia. Ilidhihirika kua msimulizi wa ndani hutumia nafsi ya kwanza kuonyesha ukaribu wake na matukio. Msimulizi wa nje husimulia matukio ambayo yeye si muhusika. Hulazimika kutumia nafsi ya tatu ilituonyesha umbali wake na matukio yanayo fanyika. Hivyo msimulizi huyu hua amefichika hivyo , msomaji hamjui.

Pia, nafsi ya kwanza inayowakilishwa na kiambishi ‘ni’, ya pili inayowakilishwa na kiambishi ‘u’ na ya tatu inayowakilishwa na kiambishi ‘a’ zimetumika kwenye diwani husika. Nafsi hizi zimetumika huku vipengele vya mazingira, matukio na wahusika vikizingatiwa. Ili kumshirikisha msomaji, utafiti umebaini kuwa nafsi ya pili ndio inayotumika. Wakati uliopo, uliopita na ujao ulitumika kutathmini aina tatu za usimuliaji

Isitoshe, kazi ya msimulizi kwenye hadithi ilidhihirishwa. Msimulizi ana jukumu la kupitisha itikadi zake kwa msomaji, kumshirikisha msomaji na kumsimulia hadithi ambalo ndilo jukumu lake kuu. Kuna viwango tofauti vya hadithi vinavyo lingana na usimulizi wa hadithi ambavyo ni; hadithi ya msingi, hadithi kuu na vijihadithi vilivyo ambatanishwa kwenye hadithi za msingi na hadithi kuu. Hadithi hizi huwa na wahusika na wasimulizi tofauti. Isitoshe, nafasi ya wakati kwenye riwaya husika ilichambuliwa. Vipengele vifuatavyo vilidumishwa;

- Jinsi matukio yalivyo pangwa
- Wakati matukio hayo yalifanyika.
- Na mara ambazo matukio hayo yalitokea.

Kulingana na uchambuzi ilidhihirika kua kipengele cha mfuatano wa matukio kwenye kuwasilisha ujumbe kimepuuzwa. Kisengere nyuma kilitumika kuelezea matukio hivyo kuongeza wakati unaotumiwa kusimulia hadithi. Hii imesababisha muda ambao msomaji atatumia kusoma hadithi kuwa mwingi, hii ilidhihirishwa kupitia kipengele cha muda.

Kuzingatia kipengele cha mara ambazo matukio yamefanyika, ilibainika kuwa kuna aina tofauti za usimulizi ambazo ni; usimulizi mosi, kwenye usimulizi huu tukio linatokea mara moja na kuzungumziwa mara moja pekee. Kwenye usimulizi banifu, tokea linatukia mara kadhaa lakini linazungumziwa mara moja tu ilhali usimulizi rudufu unahusisha tukio linatokea mara kadhaa na kuzungumziwa mara nyingi. Utafiti ulibaini kuwa matukio yanaposimuliwa mara kadhaa, jinsi maneno yalivyopangwa huweza kuwa tofauti na ya awali, miundo ya sentensi nayo haifanani lakini maana yake halisi huwa imedumishwa.

Usemi na fikra za wahusika vilichanganuliwa kwenye sura ya nne. Kuna aina tofauti za usemi, usemi halisi na usemi wa taarifa. Usemi halisi unatumia nafsi ya kwanza ‘ni’ katika uwasilishaji wake ilhali usemi wa taarifa hutumia nafsi ya tatu ‘a’. matumizi ya nafsi ya kwanza kwenye usemi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

halisi hudhihirisha ukaribu uliopo baina ya mhusika na matukio. hivyo huashiria kuwa mhusika ni msimulizi wa ndani kwani ni mhusika kwenye matukio.

Kutokana na utafiti ni bayana kwamba matumizi tofauti ya usemi na mawazo ya wahusika ni mbinu bora kwani humwezesha mwandishi kuwasilisha kazi yake kwa ubora na ubunifu usiokadirika. Pia utafiti ulidhihirisha kwamba usemi na mawazo ya wahusika huwasilishwa kwa mitindo inayofanana. Mitindo ya kuwasilisha na mawazo inaweza kubadilishwa na kuwa huru hii imesababisha kuwepo kwa usemi halisi huru, usemi wa taarifa buru, fikra halisi huru na fikra za taarifa huru. Tofauti iliyopo kati ya njia za uwasilishaji za usemi na fikra za kawaida na zile zilizo huru inatokea kwenye sarufi.

Aghalabu, mwandishi hufanya mazungumzo kati ya wahusika kuwa mafupi na kufanyika kwa haraka ili kufupisha muda wa kusimulia hadithi. ili kufanikisha hili, mwandishi hulazimika kutumia fikra na usemi wa wahusika. Kuharakisha mchakato wa usimuliaji ni kipengele muhimu kwani hupunguza kuchoka msomaji asomapo hadithi. ilibainika kuwa mara nyingi msomaji huchanganyikiwa usemi na mawazo huru vinapotumika kwani hawezi kujua anaye sema maneno ni nani, hii ni kwa sababu kishazi tangulizi huwa kimedondoshwa, hivyo huwa kunazuka aina fulani ya sintofahamu.

**Sauti na Viwango vya Usimulizi, Wakati, Usemi na Fikra za Wahusika.**

Sehemu hii inaangazia na kuchunguza wakati kama kipengele cha usimulizi kwenye *Diwani ya Akiba ya Wema*. Utafiti huu ulinuia kubaini iwapo msimulizi alishiriki au hakuwa mshiriki katika usimulizi. Isitoshe, ilibainika ikiwa msimulizi alitambulika moja kwa moja au la na ikiwa anasimulia mambo akiwa anayashiriki au la. Aidha, sehemu hii ilichunguza ni nafsi zipi kati ya tatu ambazo huwepo msimulizi alitumia katika kusimulia matukio. Pia, uchambuzi uliweza kuchanganua viwango vya usimulizi ambavyo vilikuwa sambamba na viwango vya hadithi.

Msimulizi ni kiungo ambacho huelekeza matukio au hadithi na humsogeza msomaji karibu na simulizi. Wanazuoni kama vile Genette (1980), Stanzel (1984) na Kenan (2003) wameeleza kwa mitazamo tofauti kuhusu nafasi ya msimulizi. Genette anadokeza kuwa msimulizi ana nafasi muhimu katika kuwasilisha hadithi kwa kuwa huwa na mamlaka ya kuamua njia itakayotumika kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji. Mwelekeo huu humwezesha msomaji kujihusisha na simulizi, na hivyo ni muhimu kutambua *nani anayeongea* na *nani anayezungumziwa* ili kufahamu kiini cha simulizi. Genette anaeleza kuwa kuna mitazamo miwili mikuu ya usimulizi: usimulizi wa ndani na usimulizi wa nje.

Kulingana na Stanzel (1984), kunaweza kutokea sauti katika nafasi tatu za usimulizi. Ingawa mitazamo yake inatofautiana kwa kiasi fulani na ile ya Genette, bado inabainisha uhusiano muhimu kati ya msimulizi na hadithi. Nafasi hizo ni: kwanza, nafsi ya kwanza ambapo msimulizi ni mhusika anayejihusisha moja kwa moja na matukio; pili, nafsi ya pili ambayo ni nadra na mara nyingi humhusisha msomaji moja kwa moja; na tatu, nafsi ya tatu ambapo msimulizi anaonekana kama mtaalamu wa matukio bila kushiriki moja kwa moja ndani ya hadithi.

Kenan (2003) naye anaeleza kuwa usimulizi unaweza kutokea katika viwango tofauti kulingana na nafasi ya msimulizi na matukio anayoyasimulia. Kiwango cha kwanza huhusisha msimulizi anayetoa hadithi ya msingi ambayo mara nyingi ni kisa kinachomhusu binafsi. Katika kiwango hiki, msimulizi hushiriki moja kwa moja katika hadithi na simulizi lake huzingatia uzoefu wake binafsi badala ya kuhusisha wahusika wengine.

Katika mtazamo wa usimulizi wa ndani, msimulizi hushiriki moja kwa moja katika matukio

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

yanayosimuliwa na huwa sehemu ya ulimwengu wa hadithi. Genette (1980) anaeleza kuwa usimulizi huu hutumia viwakilishi vya nafsi ya kwanza kama *mimi* ili kutoa taswira ya undani wa matukio. Wambui (2012) anaeleza kuwa matumizi ya nafsi ya kwanza huwaachia wahusika nafasi ya kujieleza na kuwasilisha hisia zao moja kwa moja mbele ya wasomaji. Mfano wa usimulizi huu unapatikana katika hadithi *Damu ya Baba* ambapo msimulizi ndiye mhusika mkuu. Anaeleza:

> *"Damu ilikuwa iinichemka. Midomo ilinicheza cheza. Sikujua nisimulie vipi kisa nilichojibidisha kukisahau bila mafanikio..."* (uk. 1).

Hapa, msimulizi anatoa taswira ya hasira na uchungu alioupitia, akisisitiza mapambano yake ya kihemko kupitia nafsi ya kwanza.

Usimulizi wa nje hutokea pale ambapo msimulizi hayumo ndani ya ulimwengu wa hadithi na badala yake huelezea matukio kwa umbali. Katika hadithi *Akiba ya Wema*, simulizi linaeleza:

> *"Alikuwa kijana mdogo wa miaka kumi na saba au kumi na minane hivi, mweupe mrefu kidogo..."* (uk. 65).

Hapa, nafsi ya tatu *a-* imetumika, jambo linalodhihirisha kuwa msimulizi anasimulia akiwa nje ya matukio.

Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, matumizi ya viambishi *ni-* au kiwakilishi *mimi* hudhihirisha mshiriki wa moja kwa moja wa matukio. Hii imejitokeza katika hadithi *Damu ya Baba* ambapo msimulizi anasema:

> *"Nilitaka kubadilisha sura na kusuta kauli ya wengi kwamba historia hujirudia. Ndiposa mimi na Solata tukaanza juhudi za kuandaa mikutano..."* (uk. 5).

Usimulizi wa nafsi ya pili humhusisha msomaji moja kwa moja na simulizi. Katika hadithi *Sifa wa Mwakiwiwi* tunasoma:

> *"Tangu utotoni mwake alikuwa mwanafunzi wa kupigiwa mfano. Usiulize alivyotia fora katika masomo..."* (uk. 13).

Hapa, kiambishi *u-* kinamshirikisha msomaji moja kwa moja.

Nafsi ya tatu hutumia kiambishi *a-* kuashiria umbali wa msimulizi na matukio. Katika hadithi *Mabega ya Mkurugenzi* tunasoma:

> *"Alimtazama mkewe kama aliyepandwa na pepo fulani..."* (uk. 90).

Hapa, msimulizi anaeleza hisia na hali ya mhusika kana kwamba ana ujuzi wa ndani, jambo linaloonyesha nafasi ya nafsi ya tatu katika usimulizi.

Hadithi pia huwasilishwa kwa kuzingatia nyakati tofauti. Kwa mujibu wa Genette (1980) na Arege (2012), kuna aina tatu kuu: wakati uliopita, uliopo na ujao. Usimulizi baada ya matukio unadhihirika katika hadithi ya *Akiba ya Wema* ambapo msimulizi anakumbuka safari yake kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha (uk. 62). Usimulizi kabla ya matukio hutumia viambishi vya wakati ujao kama *ta-* na unaonekana katika hadithi ya *Damu ya Baba* pale msimulizi anasema: *"Ninatumai kuwa ipo siku ukweli utadhihirika"* (uk. 3). Usimulizi sawia hutokea wakati wa simulizi na kitendo vinapotokea kwa pamoja, kama pale msimulizi anasema: *"Leo, miaka miwili baada ya kadhia, nimejasirika kutwaa kalamu..."* (uk. 1). Aidha, usimulizi zongomezi ni changamano kwa kuwa hujumuisha mchanganyiko wa nyakati hizi tofauti kama inavyojitokeza katika hadithi ya *Mabega ya Mkurugenzi* (uk. 90).

Watafiti kama Genette (1980) na Kenan (1983) pia wamelitazama suala la wakati kwa kuzingatia *wakati hadithi* na *wakati matini*. Wakati hadithi huhusisha mpangilio wa kikronolojia wa matukio, huku wakati matini ukizingatia muda unaochukua kusomwa na jinsi simulizi limepangwa. Mbinu za anakroni kama vile *analepsia* (marejeo ya nyuma) na *prolepsia* (marejeo ya mbele) zinatumika katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

diwani hii. Kwa mfano, *analepsia* inajitokeza katika *Mabega ya Mkurugenzi* (uk. 92) ambapo msimulizi anarudi kwenye matukio ya awali, ilhali *prolepsia* inadhihirika katika *Akiba ya Wema* (uk. 66) ambapo tukio la baadaye linatabiriwa.

Uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika pia ni kipengele muhimu cha usimulizi. Usemi halisi hujidhihirisha pale wahusika wananukuliwa moja kwa moja, kama katika hadithi *Akiba ya Wema*: *"Abiria wengine wahuni bwana. Anakula na kujifanya kaibiwa..."* (uk. 62). Usemi wa taarifa huwasilisha yaliyosemwa kwa njia ya kuripoti, mfano katika *Mabega ya Mkurugenzi* (uk. 93). Fikra halisi huwasilisha mawazo ya ndani ya mhusika, kama pale mzee katika *Akiba ya Wema* anapojisemea: *"Hapana… sio mimi…"* (uk. 62). Fikra za taarifa na taarifa huru huwasilisha mawazo kwa njia ya nafsi ya tatu au bila mipaka, mfano katika *Mabega ya Mkurugenzi* (uk. 94–95) ambapo mhusika anahoji ustaarabu wa wengine akilini mwake.

## HITIMISHO

Makala haya yalishughulikia mihimili ya kuchanganua jinsi ambavyo Sauti za usimulizi zimetumika na viwango tofauti vya usimulizi vinavyo tumika kwenye hadithi fupi viliangaziwa kwenye utafiti huu. Dhamira kuu ya mjadala huu ilidumishwa katika misingi ya kufafanua namna ambavyo sauti ya msimulizi huathiri uwasilishaji wa matukio na uelewa wa msomaji. Kupitia utafiti huu, ilionekana iwapo msimulizi alikuwa mshiriki au hakuwa mshiriki wa matukio. Isitoshe, nafsi za usimulizi zilichambuliwa kwenye sura hii. Kutokana na uchanganuzi huu, ilidhihirika kuwa msimulizi ana nafasi muhimu, hii ni kwa sababu msimulizi ni kiungo Kati ya hadithi na msomaji na ana jukumu la kuelezea matukio, kuwatambulisha wahusika pamoja na kutoa mtazamo wake kuhusu mambo mbalimbali yanayofanyika kwenye hadithi husika. Sehemu nyingine muhimu ilikuwa kuelewa uhusiano wa Wakati Kama kipengele cha usimulizi wa hadithi fupi. Dhamira kuu ilijikita katika kuonyesha namna ambavyo usimuliaji wa hadithi na wakati vinaingiliana pamoja na kutathmini iwapo mambo yanayo tendeka yamepangika kwa kuzingatia wakati ambao yanafanyika. Mpangilio wa matukio na matumizi ya anakroni ambayo huruhusu analepsia na prolepsia pia ulichunguzwa kwenye sura hii. Dhamira ya uchanganuzi huu ilikua ni kujadili namna ambavyo mbinu hizi zinachangia kwenye uundaji wa simulizi tata na kuvutia. Mjadala huu pia ulitathmini iwapo marudio ya matukio husimuliwa kwa maneno yale yale au hutumia mifumo mbalimbali ya sentensi. Sehemu ya mwisho ililenga kufanya uchambuzi kuhusu mbinu mbalimbali zinazotumika katika uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika Kama mbinu ya kupitisha ujumbe kwenye hadithi fupi. Dhamira ya msingi ya mjadal huu ilikuwa kuchanganua namna ambavyo mbinu Kama vile usemi halisi na usemi wa taarifa zianchangia kwenye ukuzaji wa tabia za wahusika na kuendeleza msuko wa matukio. Uchunguzi iliangazia jinsi matumizi ya lugha na mawazo ya wahusika yanvyoonyesha hisia na nia zao. Aidha umuhimu wa Kuchagua mbinu zinazofaa ili kuwezesha msomaji kuelewa muktadha wa hadithi kwa undani unasisitizwa.

## MAREJELEO


Arege, T. (2012). *Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa Rasi L' Guli* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Bal, M. (2004). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (3rd ed.). University of Toronto Press.

Bal, M. (1999). Narrative embedding. *Poetics Today, 2*(2), 41-59.

Barthes, R. (1975). *An Introduction to the Structural Analysis of Narrative*. Cambridge: University Press.

Fludernik, M. (2009). *An Introduction to Narratology*. Routledge.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4383

Gaita, J. (1998). *Narrative Process in the Kiswahili Novels of Kezilahabi and S.A. Mohamed* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse*. Oxford: Blackwell.

Fisher, W. R. (1984). Narration as a human communication paradigm: The case of public moral argument. *Communications monographs*, *51*(1), 1-22.

Kenan, R. (1983). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Methuen.

Kenan, R. (2002). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics* (2nd ed.). London: Routledge.

Kinara, G. (2012). *Maudhui ya UKIMWI katika Ua la Faraja na Kala Tufaha* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili: tamthilia, riwaya, na hadithi fupi* (Vol. 8). East African Publishers.

Mohochi, R. (2000). *Narratology: Concepts and Applications*. Nairobi: Acacia Publishers

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Acacia publishers

Mwongela, L. N. (2021). *Usimulizi katika Riwaya Trilojia ya Kiswahili: Mfano wa Siri Sirini* (Unpublished master's thesis).

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyambane, D. O. (2013). *The Role of Oral Literature in the Construction of the Abagusii Community's Social Values* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi.

Omutimba, C. (2015). *Usimulizi katika Riwaya za Adili na Nduguze, Walenisi na Babu Alipofufuka* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.

Ong'ondi, B. (2005). *Uhakiki wa Usimulizi katika Riwaya ya Walenisi* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi.

Propp, V. (1968). *The Morphology of the Folk Tale*. The American Folk Society and Indiana University.

Shitemi, J. (2011). *Usimulizi katika Utenzi wa Siri Li Asirali* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi.

Stanzel, F. K. (1984). *A Theory of Narrative*. Cambridge: Cambridge University Press.

Todorov, T. (1977). *Structural Analysis of Narrative*. In *The Norton Anthology of Theory and Criticism* (eds). New York: W.W. Norton & Company.

Wambui, J. (2018). *Gender Representation in Kenyan Children's Literature* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi..

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.